BROFOA
Education Is liberation

# BROTHERS FOUNT OF ACADEMY OPEN SCHOOL

BANANA UKONGA ("KILIMANI")
Reg. No: IAE/OS/0053
E-mail: brofoa@brothersacademy.ac.tz
Website: www.brothersacademy.ac.tz Mob: 0717 280 669 /0767 280 669 /0787 280 669,

## FOMU YA MAOMBI YA KUJIUNGA NA MASOMO YA : QT, RE-SITTERS KIDATO CHA NNE.

## MAELEZO YA MWANAFUNZI

MAJINA YA MWANAFUNZI

PICHA

JINA LA UKOO ..........................................................................................

JINA LA KATI ..........................................................................................

JINA LA MWANZO ..........................................................................................

JINSIA [ME] ☐ [KE] ☐

TAREHE YA KUZALIWA ..........................................MWEZI..........................MWAKA..........................

MAHALI ALIPOZALIWA : KATA ..................................WILAYA..................MKOA..........................

SHULE ALIYOSOMA ................................ KATA .....................WILAYA.................MKOA...................

ANWANI YAKE [SIMU]................................S.L.P...........................BARUA PEPE...............................

KAZI YA MWANAFUNZI KAMA NI MTU MZIMA: ..........................................................................

WASIFU WA MWANAFUNZI KIMAHUSIANO: AMEOA ☐ AMEOLEWA ☐ BADO ☐

AFYA YA MWANAFUNZI: NZURI ☐ MBAYA ☐

NAMNA ALIVYOPATA TAARIFA ZA SHULE YA BROTHERS ACADEMY:

TOVUTI ☐ TV ☐ RADIO ☐ MAGAZETI ☐

VEPEPERUSHI ☐ BANGO ☐ USHUHUDA ☐

## MAELEZO YA MZAZI/MLEZI AU MTU WA KARIBU (MDHAMINI)

JINA KAMILI: ..........................................................................................................

ANWANI YAKE: S.L.P ...........................................................SIMU: ...................................................

MAHALI ANAPOISHI KWA SASA ..................................................KAZI YAKE: ..........................................

BROFOA
Education is Liberation

**JINA LA SHULE:** BROTHERS FOUNT OF ACADEMY OPEN SCHOOL

**MAHALI ILIPO:** Shule Huria ya **BROTHERS FOUNT OF ACADEMY** inapatikana **BANANA-UKONGA(KILIMANI)**. Shule ipo njiani kabisa karibu na barabara kuu ya Pugu kwa wale wanaotoka mjini na kwingineko pande zote za mji itawalazimu washuke kituo cha daladala cha banana kisha watembee kwa mguu hatua chache kidogo baada ya jengo Mamlaka ya Anga (Aviation House) katikati ya kilima cha magereza upande wa kulia utaona bango letu na watakao shuka kituo cha magereza watatembea kuelekea Banana kwenye mteremko upande wa kushoto wataona bango letu . **BROTHERS FOUNT OF ACADEMY** ni shule huria inayofanya vizuri sana katika tasnia ya elimu katika programu za:- QT (Elimu ya sekondari kwa miaka miwili), Re -sitters (wanaorudia mitihani yao ya Sekondari kidato cha nne na sita), English course, French course na Computer course tangu ilipo anzishwa.

**FALSAFA YA SHULE:** Shule inaamini katika uwepo wa **MUNGU**, na kwamba kila kitu kinawezekana na mwenye hofu ya MUNGU pekee ndiye anayeweza kufundishika na kutimiza malengo yake kiroho na kimwili

**MALENGO YA SHULE:** Ni kumwandaa mwanafunzi ipasavyo katika nidhamu ifaayo kwa ajili ya hatua zaidi kielimu

**KAULI MBIU**: Elimu ni ukombozi

**ADA ZETU**: Ada zetu ni nafuu kabisa ukilinganisha na huduma zetu.Mwanafunzi atapaswa kulipa gharama ya fomu ya kujiunga ambayo ni Tshs. 10,000/= na ada ya kila mwezi ni Tshs. 40,000/= ambapo kwa mwaka mzima itakuwa Tshs. 480,000/=.

**UTARATIBU WA MALIPO**:

Ada hulipw**a kwa mwaka, miezi sita au miezi mitatu, kupitia**

**BENKI YA DAR ES SALAAM COMMUNITY BANK (DCB)**

**AKAUNTI NAMBA; 062010000056,**

**JINA LA AKAUNTI ; BROTHERS FOUNT OF ACADEMY OPEN SCHOOL .**

## GHARAMA NYINGINEZO:

- ✓ Mwanafunzi atapaswa kulipia gharama za majaribio/mitihani ya shule kiasi cha Tshs.50000/= kwa mwaka,ambayo hufanyika kila mwisho wa wiki kwa kipindi cha mwaka mzima .
- ✓ Mwanafunzi atalazimika kulipia gharama ya fomu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ( TEWW)ambayo ni Tshs 10000/=,pesa za co-ordination ambayo ni Tshs 20,000/= na pesa ya mtihani wa Mock Tshs 20,000/= kwa QT Hatua ya pili /Re-sitters pia Tshs 15000/= kwa QT Hatua ya kwanza

Mwanafunzi atapaswa kuja na Rimu ya karatasi nyeupe (**A4**) anapoanza masomo

- ✓ Mwanafunzi atalazimika kuchangia gharama za huduma za kijamii (Tshs 15,000) kwa mwaka

## TARATIBU NA SHERIA ZA SHULE

- ➢ Ada zetu hulipwa mwanzoni mara tu mwanafunzi anapojiunga. Na kwa wale wanaoendelea Ada hulipwa Tarehe moja ya mwezi, Utaruhusiwa kulipa kuanzia miezi mitatu, miezi sita au mwaka kupitia Dar es salaam Community Bank ( DCB ) Akaunti namba **062010000056,** Jina la Akaunti ; **BROTHERS FOUNT OF ACADEMY OPEN SCHOOL**
- ➢ Mwanafunzi atakayeruhusiwa kuingia darasani ni yule tu aliyelipa ADA kwa taratibu zilizowekwa na si vinginevyo,ili kuepusha usumbufu na lawama zisizo na sababu.
- ➢ Mwanafunzi atalazimika kutoa taarifa kwa njia ya maandishi kwa uongozi wa shule pale atakapokuwa na udhuru wowote unaomlazimu kuwa nje ya shule ili kuepuka usumbufu unaoweza kumsibu.
- ➢ Mwanafunzi atalazimika kuvaa mavazi ya heshima anapokuwa mazingira ya shule.
- ➢ Ni marufuku kwa mwanafunzi jinsia ya kike kuvaa suruali , nguo za kubana mwili pia kwa jinsia ya kiume kuvaa kofia(kapelo) shuleni .
- ➢ Simu haziruhusiwi darasani hivyo utazima au kuweka silent (kimya) uwapo darasani, maana uongozi wa shule na walimu kwa ujumla hawata vumilia utovu wowote wa nidhamu utakaosababishwa na simu.
- ➢ Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi awapo shuleni, kuonesha dalili au kufanya hivyo ni kosa litakalomwondoa shuleni na ada haitorudishwa.
- ➢ Usikivu kwa mwanafunzi pia ushirikiano wake na walimu ni suala la msingi katika maendeleo yake, hii ni kwa sababu ya kutaka mafanikio.

- Kutunza na kuheshimu mazingira ikiwa ni pamoja na mali za shule ni lazima kwa yeyote anayekuwa shuleni hapa Brothers Fount of Academy Open School.
  Ni lazima mwanafunzi atii sheria na programu zote za shule ikiwa ni pamoja na kuwa tayari kufanya mitihani kulingana na itakavyo pangwa na uongozi wa shule.
- Wanafunzi wetu wote hulazimika kufanya mitihani ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima hivyo uwe tayari kulipa gharama za fomu na gharama za mitihani ya MOCK(TEWW) Na kwa wote walio chini ya umri wa miaka 25 watachaguliwa kwenda A'Level kwa shule kwa shule za serikali kama watakuwa wamefaulu kwa viwango stahiki
- Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kuendekeza utoro maana inaweza kuwa tatizo kwake kimaendeleo na ndoto zake za elimu kufifia.Mtoro ( mtu asiyekuwa shuleni bila taarifa yoyote kwa njia ya maandishi) anaporudi shuleni anapaswa kulipa ada hata kama alikuwa haji shuleni vinginevyo asirudi kabisa iwe kwa masomo au msaada,huduma yoyote.
- Mwanafunzi haruhusiwi kufanya mgomo wa aina yoyote,au kushawishi migomo na fujo nyinginezo,akiwepo shuleni. Kufanya hivyo ni kosa litakalomsababishia kufukuzwa shule
- Mwanafunzi atalazimika kuwa darasani kwa muda wote wa vipindi na si kuzurura nje ya mazingira ya shule kinyume na maagizo ya uongozi.
- Risiti (Receipt) za malipo ndiyo gate pass ,hivyo ni mali yako na unapaswa kuwa nayo muda wote uwapo shuleni ,kupoteza,kuibiwa,kuisahau shule /ofisi haina dhamana na hilo.

BROFOA Education is Liberation

**NB:**Kumbuka hela ikiisha lipwa haita weza kurudishwa wala kuhamishiwa kwa mtu mwingine kwa namna yoyote ile,hivyo hakikisha una maamuzi thabiti kabisa kabla ya kulipa pesa yako.

**UTHIBITISHO WA MZAZI /MLEZI AU MDHAMINI**.

Mimi ...................................................................... kwa niaba ya.................................................................

Kwa hiari yangu bila kushawishiwa na mtu yeyote ninaahidi kufuata taratibu,sheria za shule na kutoa ushirikiano kadri itakavyohitajika kwa ajili ya maendeleo ya shule na mwanafunzi

**EEH!! MWENYEZI MUNGU NISAIDIE**